# TAARIFA KWA WANAHISA WA NMB UHAKIKI WA TAARIFA ZA KIBENKI NA NAMBA YA MLIPA KODI (TIN) KWA WANAHISA WA BENKI YA NMB

Ndugu mwanahisa, tunapenda kukutarifu kuwa benki ya NMB Plc inaendelea na zoezi la uhakiki wa taarifa za wanahisa wake. Hivyo basi tunaomba uboreshe taarifa za mawasiliano yako, taarifa za kibenki kwa ajili ya akaunti yako husika utakayotumia kupokea gawio pamoja na namba yako ya mlipa kodi ili kuwasilisha taarifa zako za kodi ya zuio (Withholding tax) kwa mamlaka ya kodi (TRA) kama sheria inavyoelekeza

Zoezi hili ni kwa wananahisa pekee wa NMB

i. Ambao hawajawasilisha namba ya mlipa kodi (Taxpayer Identification Number-TIN)
ii. Ambao wamebadilisha akaunti zao za kupokelea gawio na hawajaitaarifu benki (Ikiwa ni pamoja na wanahisa wapya).
iii. Ambao hawajawahi kupata gawio lolote tangu waliponunua hisa za NMB
iv. Ambao wamebadilisha namba ya simu au anuani ya makazi
v. Ambao akaunti zao zimefungwa/ zimelala (Dormant)

Tafadhali tembelea tawi la benki ya NMB lililo karibu nawe ukiwa na nakala ya kitambulisho chako (Kitambulisho cha Taifa/uraia, Mpiga Kura au hati ya kusafiria) pamoja na cheti cha hisa.

**Kwa maelezo Zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia:**

NMB Plc – Makao Makuu | Ohio/Ali Hassan Mwinyi

Ghorofa ya nne - Idara ya Fedha na Taarifa

S.L.P 9213, Dar es Salaam, Tanzania

**Barua Pepe:** Dividend_Unit@nmbbank.co.tz

**Au**

**Wasiliana nasi kupitia namba ya simu** 0222322356 au 0222322421